Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu:+255-732-979-509

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**THOMAS MGIRA**

**DHIDI YA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI NA. 003/2019**

**HUKUMU KUHUSU HOJA ZA MSINGI NA FIDIA**

**13 JUNI 2023**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU**

**Arusha, tarehe 13 Juni 2023**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (Mahakama), leo, ilitoa Uamuzi katika kesi ya Thoms Mgira dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Bwana Thomas Mgira (Mwombaji), ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye wakati akiwasilisha Maombi yake, alikuwa gerezani akisubiri kunyongwa kufuatia kukutwa na hatia ya kosa la mauaji. Alidai kuwa haki yake ya kusikilizwa kwa haki ilikiukwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Nchi Inayolalamikiwa) pale mahakama zake za ndani zilipomtia hatiani kutokana na ushahidi dhaifu, yaani kwa kutambuliwa na shahidi mmoja.

Mwombaji alidai kuwa ushahidi huo haukuwa wa kiapo na hauna uthibitisho na ulikuwa na mikanganyiko kadhaa ya msingi ambayo iliathiri kuaminika kwake. Aidha alidai kuwa Mahakama ya Rufani ya Nchi Inayolalamikiwa ilijinyima fursa ya kurekebisha makosa hayo kwa kukataa kuridhia maombi yake ya kuongezewa muda wa kuwasilisha maombi yake ya mapitio ya hukumu yake. Hivyo, Mwombaji anadai kuwa Nchi Inayolalamikiwa ilikiuka haki yake ya kulindwa kwa usawa mbele ya sheria na haki yake ya kusikilizwa kwa haki chini ya Ibara ya 3 na 7 ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu (Mkataba), mtawalia.

Nchi Inayolalamikiwa iliwasilisha pingamizi dhidi ya mamlaka ya Mahakama hii. Ilidai kuwa Mwombaji anaiomba Mahakama hiyo kukaa kama mahakama ya rufaa na kuamua masuala ya ushahidi ambayo yametolewa uamuzi na Mahakama yake ya Rufani.

Mahakama ilibainisha kwamba kwa mujibu wa Ibara ya 3(1) ya Protokali ya Kuanzisha Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (Protokali), ina mamlaka ya kuchunguza maombi yoyote yaliyowasilishwa kwake ilimradi haki ambazo ukiukwaji wake unadaiwa, zinalindwa na Mkataba au hati nyingine yoyote ya haki za binadamu iliyoridhiwa na Nchi Inayolalamikiwa.

Kuhusu madai ya Nchi Inayolalamikiwa kwamba Mahakama itakuwa inatumia mamlaka ya rufaa kwa kuchunguza msingi wa ushahidi wa hukumu ya Mwombaji, Mahakama ilibainisha kuwa haitumii mamlaka ya rufaa kuhusiana na uamuzi wa mahakama za ndani. Licha ya kwamba Mahakama hii si mahakama ya rufaa dhidi ya mahakama za ndani, ilisisitiza kwamba ina uwezo wa kutathmini uhalali wa mashauri ya ndani kuhusiana na viwango vilivyowekwa katika hati za kimataifa za haki za binadamu zilizoridhiwa na nchi husika, na hii haiifanyi kuwa mahakama ya rufaa. Hivyo, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi la Nchi Inayolalamikiwa kuhusiana na mamlaka yake.

Ingawa Pande zote mbili hazikupinga mamlaka yake ya muda, binafsi na ya eneo, Mahakama hata hivyo ilichunguza vipengele vingine vyote vya mamlaka yake na kuthibitisha kwamba ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza Maombi hayo.

Kuhusu kupokelewa kwa Maombi hayo, Mahakama ilizingatia pingamizi lililotolewa na Nchi Inayolalamikiwa, lililohusiana na hitaji la kuwasilisha Maombi ndani ya muda stahiki baada ya kumalizika kwa usuluhishi wa ndani.

Mahakama ilirejelea mamlaka yake ya kisheria kwamba uhalali wa ukomo wa muda wa kuifikia mahakama utategemea hali ya kila kesi na inapaswa kuamuliwa kwa msingi wa kesi baada ya kesi. Mahakama pia inabainisha msimamo wake kwamba utaratibu wa mapitio katika Mahakama ya Rufani ya Nchi Inayolalamikiwa unajumuisha suluhu isiyo ya kawaida ya kimahakama ambayo mwombaji halazimiki kuitumia. Hata hivyo, katika kesi ambapo mwombaji alijaribu kutumia utaratibu wa mapitio, Mahakama ilibainisha kuwa itazingatia muda ambao Mwombaji aliutumia katika kufuata utaratibu huo.

Katika kesi hii, Mahakama ilibainisha kwa mujibu wa kumbukumbu kwamba Mahakama ya Rufani iliamua rufaa ya Mwombaji tarehe 29 Aprili 2010 na tarehe 7 Septemba 2010, Mwombaji aliwasilisha maombi yake ya kuongezewa muda wa kuwasilisha maombi yake ya mapitio. Maombi ya Mwombaji, hata hivyo, yalitupiliwa mbali tarehe 19 Septemba 2013, ambayo ilikuwa ni miaka mitatu (3) baadaye. Kwa kuwa uamuzi wa Mahakama ya Rufani ulikuwa unasubiri kwa muda wa miaka mitatu (3), Mahakama iliona kwamba inaweza kudhaniwa kuwa Mwombaji alikuwa anasubiri matokeo ya maombi yake. Hivyo, Mahakama iliona ni muhimu kuzingatia kipindi hiki kwenye kukokotoa muda.

Hivyo, kuanzia tarehe ambapo Mahakama ya Rufani ilitupilia mbali maombi ya Mwombaji ya kuongezewa muda wa kutuma maombi ya mapitio, yaani, tarehe 19 Septemba 2013 hadi tarehe ambapo Mwombaji aliifikia Mahakama hii, yaani tarehe 22 Januari 2019, miaka mitano (5), miezi minne (4) na siku tatu (3) ilikuwa imepita. Mahakama, baada ya kuzingatia kwamba Mwombaji alijiwakilisha mwenyewe wakati anawasilisha Maombi mbele ya Mahakama, mfungwa aliyehukumiwa kifungo cha kunyongwa, aliyetengwa na watu wa kawaida, kuzuiliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine na kuzuiwa kupata taarifa, kulionesha kwamba uwasilishaji wa Maombi baada ya kuchelewa kwa miaka mitano (5), miezi minne (4) na siku tatu (3) ulikuwa na sababu kwa kuzingatia mazingira.

Kisha Mahakama ilijiridhisha kwamba masharti mengine ya kupokelewa yaliyowekwa katika Ibara ya 56 ya Mkataba yalitimizwa. Ilibainisha kuwa utambulisho wa Mwombaji ulioneshwa, Maombi yanaendana na Sheria Anzilishi ya Umoja wa Afrika na Mkataba; na kwamba hayakuwa na lugha ya kudhalilisha wala matusi. Mahakama pia iliona kuwa Maombi hayo hayakutokana na taarifa pekee zilizosambazwa kupitia vyombo vya habari na yaliwasilishwa baada ya kumalizika kwa usuluhishi wa ndani na kwamba Maombi hayo hayakuhusiana na kesi ambayo tayari ilikuwa imesuluhishwa kwa mujibu wa Ibara ya 56 (7) ya Mkataba. Hivyo, Mahakama iliona Maombi hayo yanakubalika.

Kuhusiana na hoja za msingi, Mahakama ilizingatia iwapo Nchi Inayolalamikiwa ilikiuka haki zilizoainishwa katika Ibara ya 3 na 7 ya Mkataba kwa kuchunguza madai matatu ya Mwombaji (i) hukumu yake ilitokana na ushahidi ambao haukuwa wa kuaminika (ii) maombi yake ya kuongezewa muda wa kuwasilisha maombi ya mapitio kwenye Mahakama ya Rufani yalikataliwa isivyo halali; (iii) tathmini iliyofanywa na mahakama za ndani kuhusu ushahidi uliomtia hatiani ilikuwa ya kibaguzi.

Kuhusiana na madai ya kwanza, haki ya kusikilizwa kwa haki inataka mtu kutiwa hatiani kwa shtaka la jinai kutokana na ushahidi wa kuaminika, Mahakama ilikubali kwamba aina au muundo wa ushahidi unaokubalika kwa madhumuni ya kutiwa hatiani unaweza kutofautiana katika taratibu tofauti za kisheria ili mradi ushahidi unatosha kuthibitisha hatia ya mtuhumiwa.

Kuhusu ushahidi wa utambulisho wa sura, Mahakama ilirejelea uamuzi wake katika kesi ya *Isiaga dhidi ya Tanzania* kwamba wakati ushahidi huo ndio msingi pekee wa kutiwa hatiani, uwezekano wowote wa makosa unapaswa kuondolewa na utambulisho wa mhusika wa uhalifu ujulikane kwa uhakika na ushahidi huo lazima uonyeshe maelezo madhubuti na thabiti ya eneo la uhalifu.

Katika kesi hii, Mahakama ilibainisha kutokana na kumbukumbu kwamba mahakama za kitaifa zilimtia hatiani Mwombaji kwa msingi wa ushahidi wa utambulisho wa sura uliotolewa

na Mashahidi watatu (3) wa Upande wa Mashtaka (PWs). Mahakama kimsingi zilitegemea ushahidi wa PW1 (binti wa mwathirika aliyefariki), ambaye alikuwa katika eneo la uhalifu wakati mama yake akiuawa na Mwombaji. Mashahidi wengine wawili walikuwa, mpelelezi wa polisi (PW2) na mtoto wa marehemu na ndugu wa shahidi wa kwanza (PW3).

Mahakama iliona kwamba mahakama za kitaifa zilitathmini mazingira ambayo uhalifu huo ulitendeka na kuzingatia hoja za Serikali na Mwombaji, ambaye aliwakilishwa ipasavyo na wakili, ili kuondoa makosa yanayoweza kutokea kuhusu utambulisho wa mhusika wa mauaji hayo. Zaidi ya hayo, mahakama za ndani pia zilichunguza utetezi wa Mwombaji kwamba hakuwa kwenye eneo la tukio na kuutupilia mbali kwa kuwa Mwombaji hakuainisha sifa za utetezi wake na hakutaka kumwita shahidi kusaidia utetezi wake. Hivyo, Mahakama iliona kwamba, jinsi mahakama za ndani zilivyotathmini ushahidi uliopelekea Mwombaji kutiwa hatiani, haikubaini kosa lolote la wazi au uvunjifu wa haki wenye madhara kwa Mwombaji.

Kuhusiana na madai ya kukataliwa ombi la kuongezewa muda wa kuwasilisha maombi ya mapitio ya uamuzi wa Mahakama ya Rufani, Mahakama inaona kwamba Mwombaji anakubali katika Maombi yake kwamba Mahakama ya Rufani ilitoa hukumu mbele yake na kwamba aliwakilishwa na wakili. Baada ya kuelewa yaliyomo katika hukumu hiyo, Mwombaji angeweza kuwasilisha notisi yake ya hoja ya mapitio ndani ya muda uliowekwa katika sheria ya nchi. Kwa mantiki hiyo, Mahakama iliona kushindwa kwa Mwombaji kuzingatia ukomo wa muda wa kuwasilisha maombi ya mapitio hayo kulitokana na kutokuwa na umakini kwa upande wake.

Kwa kuzingatia hayo, Mahakama ilihitimisha kuwa tathmini ya ushahidi katika mahakama za ndani ilifanywa kwa njia inayofaa na kwamba, kwa sababu hiyo, Mahakama imeona kuwa Nchi Inayolalamikiwa haikukiuka haki ya Mwombaji ya kushtakiwa kwa haki inayolindwa chini ya Ibara ya 7 ya Mkataba.

Kuhusu dai la tatu la Mwombaji kwamba tathmini iliyofanywa na mahakama za ndani kuhusu ushahidi uliopelekea kuhukumiwa kwake ilikuwa ya kibaguzi, hivyo basi, kukiuka haki zake chini ya Ibara ya 3 ya Mkataba huo, Mahakama ilibainisha kuwa haki ya ulinzi sawa wa kisheria inatamka kwamba “sheria itakataza ubaguzi wowote na kuwahakikishia watu wote ulinzi sawa na unaofaa dhidi ya ubaguzi kwa misingi yoyote kama vile rangi, jinsia, lugha, dini, siasa au maoni mengine, asili ya kitaifa au kijamii, mali, kuzaliwa au hali nyingine”. Mahakama pia ilibainisha kuwa haki ya usawa mbele ya sheria pia inataka watu wote wawe sawa mbele ya mahakama.

Katika Maombi haya, Mahakama iliona kwamba mahakama za kitaifa zilichunguza sababu zote za rufaa ya Mwombaji na kuona kwamba hazikuwa na hoja za msingi. Katika shauri hili, Mahakama ilibainisha kwamba haikuona chochote kwenye kumbukumbu kilichoonyesha

kwamba Mwombaji alitendewa isivyo haki au alitendewa kwa ubaguzi wakati wa shauri la ndani. Hivyo, Mahakama ilitupilia mbali madai kwamba Nchi Inayolalamikiwa ilikiuka Ibara ya 3(1) na (2) ya Mkataba.

Kuhusu fidia, Mwombaji aliiomba Mahakama impatie fidia kutokana na ukiukwaji huo alioufanyiwa ikiwa ni pamoja na kufuta hukumu yake na kuamuru aachiwe huru. Nchi Inayolalamikiwa iliiomba Mahakama kutupilia mbali maombi ya fidia, kwa kuwa Mwombaji alitiwa hatiani na kuhukumiwa kwa mujibu wa sheria. Mahakama iliona kwamba hakuna ukiukwaji uliofanyika na hivyo, ombi la fidia halikuwa na msingi tena na hivyo, ilitupilia mbali maombi ya Mwombaji kuhusiana na fidia.

Kila Upande uliamriwa kubeba gharama zake.

Kwa mujibu wa Ibara ya 28(7) ya Protokali na Kanuni ya 70(1) ya Kanuni hizi, Jaji Blaise TCHIKAYA alitoa Maoni Tofauti kwa Sehemu fulani, Jaji Ben KIOKO, Jaji Tujilane R. CHIZUMILA na Jaji Dennis ADJEI walitoa Maoni Tofauti ya Pamoja na Jaji Chafika BENSAOULA alitoa Maoni Tofauti.

**Taarifa za ziada**

Taarifa zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na nakala kamili ya hukumu ya Mahakama ya Afrika, inapatikana kwenye tovuti: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0032019

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe: registrar@african-court.org

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu ni mahakama ya bara iliyoanzishwa na nchi za Afrika ili kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu barani Afrika. Mahakama ina mamlaka kuhusiana na kesi na migogoro yote iliyowasilishwa kwake kuhusiana na tafsiri na matumizi ya Mkataba, Protokali hii na hati nyingine zozote za Haki za Binadamu zilizoridhiwa na Nchi husika. Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu: www.african-court.org.*